*Kuishi pasipo kujua kwanini unaishi na kwanini maisha yako yapo hapa duniani kunaweza kuleta utata mkubwa sana maishani mwako.*

Unatakiwa kujua kwamba, Mungu aliumba kila kitu hapa duniani kwa sababu fulani, kwa kusema hivyo kila kitu kipo hapa duniani kwa sababu kuna sababu zinazokifanya kiwepo.

Na ili kiweze kupata sababu za kuwepo kwake hapa duniani hakina budi kupata maono kamili kuhusu maisha yake.

Na ifahamike kwamba, maisha yaliyokosa maono hayana tofauti na mgodi wenye thamani kubwa sana, uliokosa mchimbaji! Ukweli ni kwamba watu wengi ni matajiri lakini hubaki kuwa maskini kutokana na kushindwa kuona kile kilichomo maishani mwao, matokeo yake hujikuta wakiishia kuuza maisha yao kwa gharama ndogo.

Na ifahamike kwamba, sizungumzii uoni unaotokana na macho ya nyama lahasha! Kwa maana unaweza kuwa na macho mawili yenye kuona vizuri lakini ukakosa maono.

Kwa sababu maono hayahusishi kile kinachoonwa na macho bali yanahusisha kile kinachoonwa nafsini mwa mtu pamoja na sababu za kuwepo kwake hapa duniani.

Namaanisha kwamba, maono ni kile ambacho mtu anakuwa anakiona kumhusu hata akiwa amefumba macho yake.

Unatakiwa kujua kwamba, maono yanayozungumziwa hapa yanamaanisha kile kitu kinachoonwa ndani ya nafsi yako, ama kwa lugha nyingine tuseme kile kitu kilichopelekea kuumbwa kwako na kuwepo kwako hapa duniani!

Ukienda kusoma maandiko matakatifu katika kitabu cha Mithali 23:7 utakutana na andiko lisemalo; *"Maana aonavyo nafsini mwake ndivyo alivyo."* Hii inamaanisha kwamba yale maono uliyonayo ndani ya nafsi yako ndiyo yatakufanya uwe vile utakavyokuwa, na hauwezi ukaenda zaidi ya pale ulipoishia kujiona.

Kwa kusema hivyo, umekuwa hivyo ulivyo na umefika hapo ulipo kutokana na maono uliyokuwa nayo na utakuwa hivi ama vile kesho kutokana na maono uliyonayo leo!

**Ukweli ni kwamba, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kusudi la maisha ya kila mwanadamu pamoja na maono aliyonayo kuhusu maisha yake. Na ifahamike kwamba, kusudi ni kufanyika kwa jambo fulani,** kwa hivi kuna kila sababu ya kufanyika na kuwepo kwa maisha yako hapa duniani.

Kwa hiyo basi kama kuna kila sababu ya kufanyika kwa maisha yako, inamaanisha kwamba, unatakiwa uanze kujiona katika vile viwango viliyofanya uumbwe hapa duniani.

Unatakiwa kujua kwamba Mungu kaweka maono ndani ya nafsi ya kila mtu, lakini kusudi la maisha yake ndilo hupima pale atakapofikia kuyaishi maono hayo.

Kumbe sasa maono ni kama injini inayofanya kazi ya kulichochea kusudi la maisha ya kila mtu hapa duniani. Kwa hiyo pasipo maono mtu anaweza asiliishi kusudi lake au akaishia kuishi sehemu ndogo tu ya kusudi lake.

Kwa mfano pasipo maono mtu anaweza kuishia kuwa mfanyakazi tu kwa kubadilishana thamani ya maisha yake na mshahara, na asifike mbali kimaisha kwa sababu hajaweza kupata maono kamili kuhusu maisha yake.

Wengi huridhika na hadhi ya kuwa wafanyakazi tu maisha yao yote, wakidhani pengine labda hayo ndiyo makusudi ya kuumbwa kwao hapa duniani kumbe huenda ikawa sio hivyo.

Hata hivyo kwa mujibu wa tafiti nyingi zilizofanyika zimeonesha kwamba wafanyakazi wengi hawazipendi kazi zao, ila hujikuta wakifanya tu kwa sababu kuna mifumo fulani iliyowatengeneza na kuwafanya wawe hivyo.

Ukweli ni kwamba maisha pasipo maono hata rasilimali zilizopo, watu na mali nyingine huwa hazina maana yoyote ile. Kwa sababu kama mtu hajapata maono kuhusu thamani ya vitu hivyo, inamaanisha kwamba hataweza kutumia vitu maono.

*Kumbe watu wengi ni maskini si kwamba wanatakiwa kuwa maskini, bali ni maskini kwa sababu wamekosa maono kuhusu maisha yao!*

Unatakiwa kujua kwamba, hakuna mtu maskini kama mtu anayeishi huku akiwa hana maono. Hata hivyo hakuna mtu ambaye huishi kwa kuchanganyikiwa maishani mwake kama mtu anayeishi huku akiwa hana maono.

Inasikitisha sana pale unakuta mtu ana kila kitu kinachoweza kumfanya kufanikiwa maishani mwake lakini akashindwa kufanikiwa kwa sababu tu ya kukosa maono.

Mtu huyu hushindwa kufika mbali kimaisha kwa sababu hana maono yanayoweza kumtoa kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine.

Kwa hivi hujikuta akishindwa kudhibiti baadhi ya mtindo wa kuishi ambao *unaweza* kumdidimiza na kumfanya ashindwe kuona thamani ya maisha yake.

Na ndiyo maana hata Mithali 29:18 neno la Mungu linasema; *"Pasipo maono watu huacha kujizuia."* Hii inamaanisha kwamba ukikosa maono kuna baadhi ya tabia, mawazo, matendo na mienendo utashindwa kuizuia kwa sababu hauna maono, kwa hivyo hutajua athari za ufanyaji wa mambo hayo katika kesho yako ijayo.

Matokeo yake utajikuta ukiharibikiwa maishani. Na hivi ndivyo wengi wetu tunavyoharibikiwa kutokana na kukosa maono.

Katika kitabu hiki utajifunza: maana halisi na chanzo cha maono ambapo kila mtu anaweza akachota maono yake huko, sababu ambazo husababisha watu wengi waishi pasipo maono, athari za kuishi bila maono, kanuni zitakazokuongoza ili uyaishi maono yako, namna ya kuyageuza maono yako na kuyafanya yawe kitu halisi kwenye maisha yako.

Ninakualika usome kitabu hiki mpaka mwisho kwa maana kimebeba jawabu tosha juu ya maswali yote uliyokuwa ukijiuliza

Ndimi Emmanuel Samuel King'unge mhitimu kutoka chuo kikuu cha Dar es salaam na mwandishi wa kitabu.